

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA
UCHAGUZI, MHE. JAJI MSTAAFU DAMIAN LUBUVA KWENYE
UFUNGUZI WA MKUTANO WA TUME NA VIONGOZI WA
VYAMA VYA SIASA KUHUSU MAADILI YA UCHAGUZI WA
RAIS, WABUNGE NA MADIWANI
TAREHE 3 JULAI, 2015 KATIKA UKUMBI WA HOTELI YA
SERENA DAR ES SALAAM**

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,
Mheshimiwa Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri
Mkuu,
Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya
Uchaguzi,
Waheshimiwa Makamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Watendaji wa Tume,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana.**

**Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,
Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Tume ya Taifa ya
Uchaguzi, kuwakaribisheni wote katika mkutano huu muhimu**

wa kujadili Maadili ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2015.

Ninatambua kuwa mnayo majukumu mengi na ya muhimu lakini mmeona ni muhimu kufika hapa kuhudhuria mkutano huu kama ilivyotarajiwa. Asanteni na karibuni sana.

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Mtakubaliana nami kuwa kupiga kura ni haki ya msingi na ya kikatiba kwa kila raia wa Tanzania. Hivyo, Uchaguzi unapaswa kuwa huru, wa haki, uwazi na wa kuaminika. Aidha, Amani, Ustawi wa nchi, Usalama wa Raia, uhuru wa Vyama vya Siasa na utii wa Sheria, Kanuni na taratibu za uchaguzi ndiyo msingi wa uchaguzi ulio huru, haki na unaozingatia ushiriki wa makundi yote ya jamii katika uchaguzi.

Napenda niwahakikishie ninyi Viongozi wa vyama vya Siasa na Umma wa Watanzania kwamba Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 utafanyika kwa Haki na Uhuru na kwa mara nyingine niwahakikishie zoezi hili litafanyika kwa uangalifu mkubwa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu kama ambavyo hivi leo tunakutana kuzungumzia suala la Maadili ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Aidha, Maadili haya yatahusisha zaidi Vyama vya Siasa, wagombea wote, Serikali pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na yanazungumzia wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea. Kwa mfano, kila chama na mgombea atatakiwa kuheshimu na kutekeleza Sheria za Uchaguzi, Kanuni, Maadili na Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi, yaani kipindi chote cha Kampeni, kuanzia siku moja baada ya uteuzi hadi siku ya Uchaguzi, Oktoba 2015.

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Maadili haya tutakayoyajadili leo yatahusisha mambo mbalimbali yasiyotakiwa kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea wao kama vile kufanya fujo au kusababisha vurugu ya aina yoyote katika mkutano wa Chama kingine cha Siasa. Maadili yatakayotakiwa kuzingatiwa wakati wa upigaji kura mpaka kutangaza matokeo ya Uchaguzi ni pamoja na

viongozi wa Vyama vya Siasa kuwaelimisha wafuasi wao kuondoka vituoni mara tu baada ya kupiga kura ili kuepusha msongamano na vitendo vingine vinavyoweza kuchochea kuvunjika kwa amani.

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Wajibu wa Serikali wakati wa Uchaguzi ni kutoa fursa sawa kwa wadau wote vikiwemo Vyama vya Siasa ili kuviwezesha kuendesha shughuli zao za kisiasa kwa kuzingatia sheria za nchi. Katika Mkutano wetu wa leo tutajadili kwa mapana Maadili ya Uchaguzi na utekelezaji wake. Itakumbukwa kuwa kabla ya Uchaguzi mkuu wa mwaka 2010, tulikutana kwa namna hii na kujadili maadili ya uchaguzi na kuyatekeleza kwa pamoja. Pia naomba niwahakikishie kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaendesha zoezi la Uchaguzi kwa kuzingatia Katiba ya nchi ambayo ni Sheria mama, Sheria za Uchaguzi, Sheria nyingine za nchi, kanuni na Maadili ya Uchaguzi. Mengi zaidi tutashirikishana katika Maadili tunayojadili katika mkutano huu muhimu.

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Madhumuni ya Maadili ya Uchaguzi ni kuhakikisha Wadau wa Uchaguzi hasa Vyama Vya Siasa, Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wanatekeleza majukumu yao katika hali ya amani na utulivu.

Maadili haya yanalenga kueleza yanayotakiwa kufanywa na yasiyotakiwa kufanywa na wahusika hawa wa Maadili. Aidha, kwa kuwa Maadili haya yanaundwa kwa mujibu wa sheria, basi yameweka utaratibu wa kuyatekeleza ikiwa ni pamoja na uundwaji wa kamati za Maadili kuanzia ngazi ya Kata, Jimbo, Taifa na Rufaa.

Pia, Maadili yanaainisha namna na muda wa kuwasilisha malalamiko ya ukiukwaji wa Maadili. Adhabu kwa watakaokiuka Maadili pia ni sehemu ya Maadili.

Ni rai ya Tume kwenu nyote tujadili Maadili haya katika weledi wetu ili tupate mwongozo utakaotuongoza kipindi chote cha Kampeni na siku ya Uchaguzi. Kila Mhusika wa

Maadili haya ana uhuru wa kuchangia mawazo yake na yataheshimiwa.

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kwa kumalizia, ninapenda tena kuwashukuru wote kwa kuhudhuria mkutano huu. Ombi letu kwenu ni kwamba tutoe michango ya kufanikisha Maadili haya pia msaidie kuwahamasisha wananchi na wafuasi wenu kuheshimu Maadili na sheria nyingine za uchaguzi na waweze kujitokeza kwa wingi kwenye zoezi la kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 25 mwaka huu.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA